

TANGAZO KWA UMMA

MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJI KUTOKA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA MJI WA LINDI (“Lindi WSSA”) KWA MWAKA 2018/19 – 2020/21

Maombi ya mabadiliko ya Bei Na. TR-W-18-019-2018

Mnamo tarehe 12 Julai 2018, Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea ombi kutoka kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Mji wa Lindi (Lindi WSSA) la kutaka kurekebisha bei ya huduma zake za majisafi kwa mwaka 2018/19 hadi 2020/21 na kuanzisha huduma ya uondoaji Majitaka. Jedwali namba 1 hadi 6 hapa chini yanaonesha mchanganuo wa bei za sasa na zinazopendekezwa.

Jedwali 1: Bei za Maji za sasa na zinazopendekezwa (shilingi kwa mita moja ya ujazo)

Aina ya Mteja	Matumizi (Mita za Ujazo)	Bei za sasa	Bei zilizopendekezwa					
		2017/18	% Badiliko	2018/19	% Badiliko	2019/20	% Badiliko	2020/21
Majumbani	0-5	950	89%	1,800	6%	1,900	0%	1,900
	>5-10	950	95%	1,850	5%	1,950	3%	2,000
	>10	1,220	39%	1,700	1%	1,710	0%	1,715
Taasisi		1,100	118%	2,400	4%	2,500	0%	2,500
Biashara		1,400	79%	2,500	4%	2,600	0%	2,600
Viwanda		1,600	56%	2,500	4%	2,600	0%	2,600
Magati	Ndoo ya lita 20	1,000	100%	2,000	0%	2,000	0%	2,000
Wateja wa Jumla	Mita za Ujazo	2,300	96%	4,500	0%	4,500	0%	4,500

Jedwali 2: Tozo za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma ya Maji Baada ya Kusitishwa (Shilingi kwa marejesho)

Aina za Wateja	Bei za Sasa	Bei zinazopendekezwa					
	2017/18	% Badiliko	2018/19	% Badiliko	2019/20	% Badiliko	2020/21
Majumbani	10,000	0%	10,000	0%	10,000	0%	10,000
Taasisi	40,000	0%	40,000	0%	40,000	0%	40,000
Biashara	40,000	0%	40,000	0%	40,000	0%	40,000
Viwandani	40,000	0%	40,000	0%	40,000	0%	40,000

Jedwali 3: Tozo za Sasa na Zinazopendekezwa za Maunganisho Mapya (Shilingi kwa maunganisho mapya)

Customer Category	Bei za Sasa	Bei zinazopendekezwa				
	2017/18	2018/19	% Change	2019/20	% Change	2020/21
Majumbani	30,000	25% ya gharama za vifaa vya maunganisho				
Taasisi	40,000					
Biashara	40,000					
Viwandani	40,000					

Jedwali 4: Tozo za Huduma za Sasa na zilizopendekezwa (Shilingi/mwezi)

Aina za Wateja	Bei za sasa	Tozo zilizopendekezwa kwa miaka mitatu			
	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21	
Majumbani	2,500	0	0	0	
Taasisi	2,500	0	0	0	
Biashara	2,500	0	0	0	
Viwandani	3,400	0	0	0	

Jedwali 5: Mapendekezo ya Bei kwa Wateja Wasio na Dira (Shilingi/Mwezi)

Aina za Wateja	Bei za Sasa	Bei zilizopendekezwa kwa kipindi cha miaka mitatu					
	2017/18	Badiliko	2018/19	Badiliko	2019/20	Badiliko	2020/21
Majumbani	9,000	94%	17,500	3%	18,000	3%	18,500
Taasisi	19,000	111%	40,000	13%	45,000	44%	65,000
Biashara	32,000	25%	40,000	13%	45,000	44%	65,000
Viwandani	42,000	90%	80,000	6%	85,000	6%	90,000

Jedwali 6: Mapendekezo Mapya ya Bei za Huduma ya Majitaka (Shilingi/Mita za Ujazo)

Aina za Wateja	Bei zilizopendekezwa				
	2018/19	% Badiliko	2019/20	% Badiliko	2020/21
Majumbani	10,000	0%	10,000	0%	10,000
Taasisi	20,000	0%	20,000	0%	20,000
Biashara	20,000	0%	20,000	0%	20,000
Viwandani	20,000	0%	20,000	0%	20,000

Kutokana na wasilisho la Lindi WSSA, bei zinazopendekezwa zitaiwezesha Mamlaka kumudu ongezeko la gharama za uendeshaji kutokana na kukamilika kwa mradi wa maji wa Ngápa, kupata fedha kuongeza uwekezaji ili kupanua huduma zake ziweze kuwafikia wananchi walio wengi zaidi na kuboresha utoaji wa huduma ya maji safi katika mji wa Lindi.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Jumatano, tarehe 3 Oktoba, 2018, katika Double M, Lindi Mjini** kuanzia saa **4:00 asubuhi** kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali, Baraza la Ushauri la watumia Huduma zinazodhibitiwa na EWURA na wananchi wote kwa ujumla, kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyooneshwa hapo juu ndani ya kipindi kabla ya tarehe **10 Oktoba, 2018**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana Makao Makuu ya EWURA, **GHOROFA YA NNE, JENGO LA LAPF, BARABARA YA MAKOLE, DODOMA** au ofisi za Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Mji wa Lindi zilizopo Barabara ya Dar es Salaam/Lindi, Mkabala na Shule ya Sekondari Lindi.

Imetolewa Na
Kaimu Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)